05

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## MEI, 2026

**26 JUNI, 2026**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI,2026

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.

## LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA YALIYORIPOTIWA POLISI MEI 2026

Jumla ya matukio 128 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2026 ambapo waathirika walikuwa 128. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 109 sawa na asilimia 85.2), wakifuatiwa na wanawake 17 (asilimia 13.3) na wanaume wawili (2) sawa na asilimia 1.6.


Miongoni mwa waathirika watoto 109, wasichana walikuwa 96 (asilimia 88.1) na wavulana walikuwa 13 sawa na asilimia 11.9 ya waathirika watoto wote.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia, Mei 2026**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 65, ambapo waathirika 60 walikuwa wasichana na watano (5) wanawake. Tukio la kujaribu kubaka lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamke. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa tisa (9) ambapo waathirika wote walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 10 ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha yalikuwa 11 ambapo waathirika 10 walikuwa wasichana na mwathirika mmoja (1) alikuwa mwanamke. Matukio ya lugha ya matusi yalikuwa 13 ambapo waathirika watano (5) walikuwa wanawake, waathrika watatu (3) wasichana, waathirika wanne (4) walikuwa wavulana na mwathirika mmoja (1) mwanamme. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 15 ambapo waathirika wanne (4) walikuwa wanawake, waathirika 10 walikuwa wasichana na mwathirika mmoja (1) alikuwa ni mwanamme. Tukio la kutelekeza watoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika ni wavulana. Tukio la kutupa watoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa msichana, tukio la ukatili wa mtoto/mtu mwenye ulemavu lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa ni msichana, na tukio ya kumpa na kupokea ujauzito lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamke.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Mei, 2026**



Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa matukio mengi, matukio 25 sawa na asilimia 19.5 ikifuatia Wilaya ya Magharibi ‘B’ ambayo imeripotiwa matukio 24 (asilimia 18.8). Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio mawili (2) sawa na asilimia 1.6 ya matukio yote yaliyoripotiwa.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2026**



Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 0.8 kufikia matukio 128 kwa mwezi Mei, 2026 ikilinganishwa na matukio 129 yaliyoripotiwa mwezi wa Aprili, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Mei, 2026 yalikuwa matukio ya kujaribu kubaka, kutupa watoto, kuingilia kinyume na maumbile, lugha ya matusi, shambulio la aibu/kukashifu na shambulio la mtoto. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa(matukio 25) ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2026 na Wilaya ya Mjini iliongoza kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Aprili, 2026 (matukio 25).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili 2026 na Mei, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kutupa Watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 |
| Kaskazini 'A' | 8 | 6 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 8 | 5 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 10 | 13 | 8 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mjini | 25 | 20 | 12 | 10 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 23 | 25 | 8 | 7 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 3 | 3 | 4 | 5 |
| Magharibi 'B' | 21 | 24 | 8 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 | 3 | 4 | 2 | 2 |
| Wete | 9 | 12 | 6 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 3 | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 6 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 |
| Mkoani | 10 | 8 | 7 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **129** | **128** | **67** | **65** | **0** | **1** | **0** | **1** | **9** | **9** | **8** | **10** | **15** | **11** |

**Inaendelea....Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili 2026 na Mei, 2026**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya Matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Watoto | | Mauaji | | Uzinifu | | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Shambulio la Mtoto | |
| | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 | Aprili 2026 | Mei 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 4 | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 3 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **10** | **13** | **12** | **15** | **1** | **1** | **2** | **0** | **1** | **0** | **4** | **1** | **0** | **1** |

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 19.6 na kufikia matukio 128 kwa mwezi Mei, 2026 kutoka matukio 107 yaliyoripotiwa mwezi wa Mei, 2025. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Mei, 2026 isipokuwa matukio ya kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, mauaji na wizi wa watoto. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa Mei, 2026 (matukio 25) na mwezi wa Mei, 2025 (matukio 23).

**Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mei 2025 na Mei 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kujaribu Kubaka | | Kutupa Watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | |
| | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 |
| Kaskazini 'A' | 8 | 6 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 8 | 3 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 16 | 13 | 12 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini | 5 | 2 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 18 | 20 | 12 | 10 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 23 | 25 | 13 | 7 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 5 | 3 | 1 | 5 |
| Magharibi 'B' | 22 | 24 | 14 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 3 | 4 | 2 | 2 |
| Wete | 4 | 12 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Micheweni | 3 | 4 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 6 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mkoani | 2 | 8 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **128** | **68** | **65** | **0** | **1** | **0** | **1** | **9** | **9** | **12** | **10** | **11** | **11** |

**Inaendelea....Jadweli 1.3: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mei 2025 na Mei 2026**

| Wilaya | Aina ya Matukio ya Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Lugha ya Matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza watoto | | Mauaji | | Wizi wa Watoto | | Kumpa na Kupokea Ujauzito | | Shambulio la Mtoto | |
| | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 | Mei-2025 | Mei-2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 4 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 3 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **0** | **13** | **4** | **15** | **0** | **1** | **2** | **0** | **1** | **0** | **0** | **1** | **0** | **1** |

Miongoni mwa waathirika watoto 109 waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 60, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana tisa (9), kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 10, kutorosha walikuwa wasichana tisa (9), shambulio la aibu/kukashifu wasichana walikuwa 10, lugha ya matusi wasichana watatu (3) na wavulana wanne (4), kutelekeza watoto alikuwa msichana mmoja (1), kutupa watoto alikuwa msichana mmoja (1) na Shambulio la mtoto alikuwa msichana mmoja (1).

**Jadweli 1.4: Idadi ya Matukio na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mei, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Watoto | | Kutupa Watoto | | Shambulio la Mtoto | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 6 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 12 | 9 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 17 | 8 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 19 | 6 | 2 | 3 | 4 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 22 | 10 | 3 | 4 | 2 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 8 | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 7 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **109** | **60** | **9** | **10** | **9** | **0** | **3** | **4** | **10** | **0** | **1** | **0** | **1** | **0** | **1** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 17 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa watano (5),Kujaribu kubaka alikuwa mmoja (1), Kutorosha alikuwa mmoja (1), Lugha ya matusi watano (5), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wanne (4) na Kumpa na kupokea ujauzto alikuwa mmoja (1).

**Jadweli 1.5: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mei, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya udhalilishaji | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kutorosha | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Kumpa na Kupokea ujauzito | Uzinifu |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **17** | **5** | **1** | **1** | **5** | **4** | **1** | **0** |

Kwa mwezi wa  Mei 2026, idadi ya waathirika wanaume walikuwa ni wawili (2), mwathirika mmoja (1) wa tukio la Lugha ya matusi na mwathirika mmoja (1) tukio la shambulio la aibu.

**Jadweli 1.6: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mei, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya udhalilishaji | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti/Kunajisi | Lugha ya matusi | Shambulio la aibu/Kukashifu | Mauaji | Kumpa na Kupokea ujauzito | Wizi wa watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 70) sawa na asilimia 64.2 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 22) sawa na asilimia 20.2. Matukio 11 sawa na asilimia 10.1 yaliripotiwa kwa umri wa miaka 6-10 na umri wa miaka 0-5, yaliripotiwamatukio sita (6) sawa na asilimia 5.5. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 48) sawa na asilimia 80.0 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.7: Aina ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Mei, 2026**

| **Umri** | **0-5** | | **6-10** | | **11-14** | | **15-17** | | **Jumla** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 0 | | 0 | | 12 | | 48 | | 60 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 1 | | 6 | | 2 | | 0 | | 9 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 3 | | 7 | | 10 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 8 | 0 | 10 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 1 | 3 | 3 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 2 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 10 | 0 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **5** | **1** | **5** | **6** | **19** | **3** | **67** | **3** | **96** | **13** |

Idadi ya matukio ya watoto waliopitia udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 0.9 kufikia matukio 109 kwa mwezi wa Mei 2026 ikilinganishwa na matukio 108 yaliyoripotiwa mwezi wa Aprili 2026. Matukio mengi yameripotiwa kuongezeka kwa watoto mwezi Mei 2026 isipokuwa matukio ya kubaka na kutorosha.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Aprili, 2026 na Mei, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kutupa watoto | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Lugha ya matusi | | Kutelekeza watoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 | Aprili - 26 | Mei - 26 |
| 0-5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 4 | 6 |
| 6-10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 6 | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 11 |
| 11-14 | 12 | 12 | 0 | 0 | 3 | 2 | 4 | 3 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 24 | 22 |
| 15-17 | 47 | 48 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 7 | 11 | 8 | 1 | 3 | 6 | 4 | 0 | 0 | 68 | 70 |
| **Jumla** | **63** | **60** | **0** | **1** | **8** | **9** | **8** | **10** | **13** | **10** | **8** | **10** | **7** | **7** | **1** | **1** | **108** | **109** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 16.0 na kufikia matukio 109 kwa mwezi wa Mei 2026 ikilinganishwa na matukio 94 yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Mei 2025. Matukio yaliyoripotiwa kupungua kwa mwezi Mei 2026 ikilinganishwa na Mei 2025 ni matukio ya kubaka,kutorosha na wizi wa watoto.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Mei, 2025 na Mei, 2026**

| Miaka | Kubaka | | Kulawiti/Kunajisi | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Lugha ya matusi | | Kutelekeza watoto | | Wizi wa watoto | | Kutupa watoto | | Shambulio la mtoto | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 | Mei - 25 | Mei - 26 |
| 0-5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 6 |
| 6-10 | 7 | 0 | 2 | 6 | 7 | 0 | 0 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 11 |
| 11-14 | 14 | 12 | 5 | 2 | 1 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 22 |
| 15-17 | 40 | 48 | 1 | 0 | 1 | 7 | 8 | 8 | 0 | 3 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 50 | 70 |
| **Jumla** | **62** | **60** | **9** | **9** | **10** | **10** | **11** | **10** | **2** | **10** | **0** | **7** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | **1** | **0** | **1** | **94** | **109** |

Matukio mengi (matukio 66) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 51.6 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 19) sawa na asilimia 14.8 na vichakani (matukio 18) sawa na asilimia 14.1 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Mei 2026.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Mei, 2026**





Matukio 113 kati ya matukio 128 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 88.3 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 11 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 8.6), matukio mawili (2) yapo mahakamani (asilimia 1.6), tukio moja (1) limefungwa na polisi (asilimia 0.8) na tukio moja (1) limepewa hati ya mashtaka (asilimia 0.8).

**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mei, 2026**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika: Watoto | | Waathirika: Watu Wazima | | Hatua Zilizofikia | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi | Hati ya Mashtaka |
| Kubaka | 65 | 60 | | 5 | | 0 | 0 | 0 | 1 | 7 | 57 | 0 |
| Kujaribu Kubaka | 1 | 0 | | 1 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kulawiti/Kunajisi | 9 | | 9 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 10 | 10 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 8 | 0 |
| Kutorosha | 11 | 10 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 |
| Lugha ya matusi | 13 | 3 | 4 | 5 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 15 | 10 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 13 | 1 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Ukatili wa mtoto/Mtu wenye ulemavu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **128** | **96** | **13** | **17** | **2** | **2** | **0** | **0** | **1** | **11** | **113** | **1** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Mei 2026 walikuwa 128 kati yao 51 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 39.8, watu wasiojulikana walikuwa 38 sawa na asilimia 29.7, Jirani walikuwa 35 sawa na asilimia 27.3, baba/mama mzazi walikuwa watatu (3) sawa na asilimia 0.8 na watu wengine alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.8

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mei, 2026**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR MEI, 2026

Jumla ya Majalada 42 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Mei, 2026 ambayo yalihusisha makosa 46. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 25) sawa na asilimia 54.3 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Mei, 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 6 | 7 |
| Kusini Unguja | 4 | 4 |
| Mjini Magharibi | 23 | 25 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 3 |
| Kusini Pemba | 6 | 7 |
| Makao Makuu | 0 | 0 |
| **Jumla** | **42** | **46** |

Kati ya Majalada 42 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Mei, 2026, majalada 13 hayajatolea uamuzi, majalada 11 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 15 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada matatu (3) yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Mei 2026**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 6 | 3 | 0 | 0 | 3 |
| Kusini Unguja | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini Magharibi | 23 | 4 | 1 | 9 | 9 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 6 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **42** | **15** | **3** | **11** | **13** |

Miongoni mwa makosa 46 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 27) sawa na asilimia 58.7 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Mei 2026**

| Mkoa | Jumla ya makosa kwenye majalada yaliopokelewa | Kutorosha | Kubaka | Kumuingilia maharimu | Kula witi | Shambulio la aibu/kukashifu | Kuingilia kinyume na maumbile |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 7 | 1 | 5 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini Unguja | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 25 | 0 | 14 | 0 | 1 | 2 | 8 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 7 | 3 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Makao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **46** | **4** | **27** | **0** | **3** | **4** | **8** |

## MASHAURI NA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI 2026

Jumla ya mashauri 15 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Mei, 2026, ambapo yamehusisha makosa 16 . Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri saba (7) yaliyohusisha makosa saba (7) sawa na asilimia 46.7 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Mei, 2026**




Kati ya mashauri 15 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri 14 bado yanaendelea na shauri moja (1) limefutwa.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Mashauri ya Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Mei 2026**

| Aina ya makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa hatiani | | | | | Zisizo na hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachiwa huru | Zilizondoshwa /Zilozfutwa |
| kubaka | 9 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| kutorosha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| kubaka mgonjwa wa akili | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **15** | **14** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **1** |

Jumla ya makosa 16 yaliyopokelewa katika Mahakama za udhalilishaji wa kijinsia, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 9) sawa na asilimia 56.3 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa Mei, 2026**

| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kubaka | 3 | 0 | 4 | 0 | 2 | 9 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kulawiti | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| kutorosha+kubaka | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| kubaka mgonjwa wa akili | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **3** | **0** | **7** | **2** | **4** | **16** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 128 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2026 ambapo waathirika walikuwa 128. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 109 sawa na asilimia 85.2), wakifuatiwa na wanawake 17 (asilimia 13.3) na wanaume wawili (2) sawa na asilimia 1.6.

Idadi ya matukio ya udhalilishaji kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 0.8 kufikia matukio 128 kwa mwezi Mei, 2026 ikilinganishwa na matukio 129 yaliyoripotiwa mwezi wa Aprili, 2026. Matukio yaliyoripotiwa kuongezeka kwa mwezi Mei, 2026 ni matukio ya kujaribu kubaka, kutupa watoto, kuingilia kinyume na maumbile, lugha ya matusi, shambulio la aibu/kukashifu na shambulio la mtoto. Wilaya ya Magharibi ‘A’ imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2026 ambapo pia wilaya ya Mjini iliripotiwa kuwa na idadi sawa ya matukio kwa mwezi wa Aprili, 2026 (matukio 25) kwa kila wilaya.

Matukio 113 kati ya matukio 128 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 88.3 ya matukio yote yaliyoripotiwa, aidha matukio 11 yamepelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (asilimia 8.6), matukio mawili (2) yapo mahakamani (asilimia 1.6), tukio moja (1) limefungwa na polisi (asilimia 0.8) na tukio moja (1) limepewa hati ya mashtaka (asilimia 0.8).

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Mei, 2026**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Majumba mabovu | | Vichakani | | Vyombo vya usafiri(Gari) | | Sehemu nyengine | | jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 0 | | 39 | | 1 | | 9 | | 15 | | 0 | | 1 | | 65 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 3 | | 0 | | 4 | | 1 | | 0 | | 1 | | 9 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 6 | | 0 | | 4 | | 0 | | 0 | | 0 | | 10 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 |
| Lugha ya matusi | 5 | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 5 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 14 | 1 |
| Kutelekeza mtoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **13** | **4** | **61** | **5** | **3** | **0** | **15** | **4** | **17** | **1** | **1** | **0** | **3** | **1** | **113** | **15** |

## Jadweli 2.0: Idadi ya Waaathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2026

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kumtelekeza mtoto | | Kutupa Watoto | | Shambulio la mtoto | | Kumpa na Kupokea ujauzito | |
| | | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'ke | W' me | W'ke | W' me | W'ke | W' me | W'ke | W' me | W'ke | W' me | W'ke | W'me | W'ke | W' me |
| Kaskazini 'A' | 6 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 13 | 9 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 20 | 10 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 25 | 7 | 1 | 2 | 3 | 5 | 0 | 2 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 24 | 10 | 0 | 3 | 4 | 2 | 0 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 12 | 7 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 8 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **128** | **65** | **1** | **9** | **11** | **10** | **0** | **8** | **5** | **14** | **1** | **1** | **0** | **1** | **0** | **1** | **0** | **1** | **0** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Aprili, 2026 na Mei, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Aprili-2026 | Mei-2026 | Aprili-2026 | Mei-2026 | Aprili-2026 | Mei-2026 | Aprili-2026 | Mei-2026 | Aprili-2026 | Mei-2026 |
| Kubaka | 67 | 65 | 4 | 5 | 63 | 60 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 9 | 9 | | | | | 8 | 9 | 1 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 8 | 10 | 0 | 0 | 8 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 15 | 11 | 1 | 1 | 13 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 10 | 13 | 3 | 5 | 3 | 3 | 4 | 0 | 0 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 12 | 15 | 4 | 4 | 6 | 10 | 2 | 0 | 0 | 1 |
| Kutupa watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Ukatili wa mtoto/Mtu wenye ulemavu | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Uzinifu | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 4 | 1 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **129** | **128** | **19** | **17** | **93** | **96** | **15** | **13** | **2** | **2** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio  na Waathirika wa Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mei, 2025 na Mei, 2026**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Mwanamme | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 | Mei-2026 |
| Kubaka | 68 | 65 | 6 | 5 | 62 | 60 | | | | |
| Kujaribu kubaka | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | | | | |
| Kulawiti/Kunajisi | 9 | 9 | | | | | 9 | 9 | 0 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 12 | 10 | 2 | 0 | 10 | 10 | | | | |
| Kutorosha | 11 | 11 | 0 | 1 | 11 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 13 | 0 | 5 | 0 | 3 | 0 | 4 | 0 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 15 | 2 | 4 | 2 | 10 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kutupa watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Ukatili wa mtoto/Mtu wenye ulemavu | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wizi wa watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutelekeza watoto | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **107** | **128** | **10** | **17** | **86** | **96** | **9** | **13** | **2** | **2** |

## Jadweli 5.0 : Idadi ya Waathirika  Wanawake na Wanaume wa Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Mei 2026

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** |
| Kubaka | 4 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 5 | |
| Kujaribu Kubaka | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kujaribu kulawiti/Kunajisi | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 |
| Kutorosha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Lugha ya matusi | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 5 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **14** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | **2** | **0** | **0** | **1** | **17** | **2** |

## Jadweli 6.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea; Mei, 2026

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** |
| Kubaka | 4 | | 6 | | 9 | | 14 | | 27 | | 4 | | 1 | | 0 | | 65 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 0 | | 2 | | 2 | | 2 | | 1 | | 0 | | 0 | | 9 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 1 | | 3 | | 5 | | 1 | | 0 | | 0 | | 10 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 |
| Lugha ya matusi | 1 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 5 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 2 | 0 | 6 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 1 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Ukatili wa mtoto/Mtu wenye ulemavu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi zaidi Tafadhali Wasiliana na:-**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**